TANGAZO LA SERIKALI NA. 282 la tarehe 7/4/2023

SHERIA YA MIPANGOMIJI

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA KWACHAGA, SUWA NA MKOMBA YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo La Kwachaga, Suwa na Mkomba ya mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa jumla na kina

3. Mipango ya jumla na ya kina katika eneo la kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo -

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenye majira - nukta 411302MS, 9365406KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 7.6 katika uelekeo wa 289° 51' 08'' hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B yenye majira - nukta 404101MS, 9368006KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini- Mashariki kwa umbali wa kilomita 4.5 katika uelekeo wa 321° 53' 15'' hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C yenye majira - nukta 401304MS, 9371571KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 3.2 katika uelekeo wa 311° 49' 33'' hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D yenye majira - nukta 398905MS, 9373717KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini -Magharibi kwa umbali wa kilomita

*Tangazo la Serikali Na. 282 (linaendelea)*

5.74 katika uelekeo wa 53° 02’ 08’’ hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba E yenye majira - nukta 403432MS, 9377123KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 4.56 katika uelekeo wa 67° 14’ 28’’ hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba F yenye majira - nukta 407634MS, 9378908KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 2.76 katika uelekeo wa 178° 12’ 53’’ hadi kwenye alama ya mpaka wa upimaji namba G yenye majira - nukta 407794MS, 9376260KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa kufuata uelekeo wa mto Wimba hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H yenye majira - nukta 414227MS, 9371990KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 2.79 katika uelekeo wa 172° 23’ 57’’ hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenye majira – nukta 411302MS, 9365406KZ; hadi ulipoanzia”.

Dodoma,
17 Machi, 2023

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*